

WAKALA WA VIPIMO (WMA)

UHAKIKI WA MALORI YA MAFUTA PAMOJA NA HAKI NA WAJIBU WA DEREVA ANAYESAFIRISHA MAFUTA.



Wakala wa Vipimo (WMA) ni mojawapo ya Wakala za Serikali ambayo ilianzishwa tarehe 13 Mei, 2002 kwa Tangazo la Serikali namba 194 la tarehe 17 Mei, 2002. Awali, ilikua ni Kitengo chini ya Idara ya Biashara Wizara ya Viwanda na Biashara. Lengo la Serikali kuanzisha Wakala wa Vipimo ni kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

DIRA

Kufikia viwango vya kimataifa katika utoaji Huduma kwa jamii kupitia matumizi sahihi ya Vipimo.

DHIMA

Kuthibiti vipimo vyote vinavyotumika na vinavyokusudiwa kutumika katika sekta ya biashara, mazingira, usalama na afya na kuelimisha umma kuhusu masuala ya vipimo nchini kwa lengo la kumlinda mlaji.

HATUA ZINAZOZINGATIWA WAKATI WA UPIMAJI WA MALORI YA MAFUTA

- i. Gari kufikishwa katika Ofisi ya Wakala wa Vipimo.
- ii. Gari kukaguliwa kwa kuangalia vigezo muhimu vinavyotakiwa kwa ajili ya upimaji.



*Afisa Vipimo
akikagua tenki
la gari ya
kusafirishia
mafuta kabla ya
upimaji.*

- iii. Gari likikidhi vigezo litasajiliwa na kuweka kumbukumbu zake sahihi.
- iv. Gari litakalokidhi vigezo litapimwa kwa kufuata hatua zote stahiki.

- v. Afisa atatakiwa kufanyakazi kwa uwazi na kumhusisha mhusika (mwenye gari) katika kila hatua ya upimaji.
- vi. Gari linapelekwa katika sehemu maalum ya upimaji (*calibration bay*) kwa ajili ya kupimwa.



Sehemu maalum
ya kupimia magari
ya mafuta katika
Mkoa wa Ilala
(*Calibration bay*).

- vii. Kuweka alama kwenye *dip stick* kwa kutumia namba na *letter punch* ili mteja ajue ujazo sahihi wa gari yake mfano, kwa kulinganisha chati atakayopewa na alama za kwenye *dip stick*.



Afisa vipimo
akiweka alama
kwenye *dip stick*
baada ya
kupimwa.

- viii. Kuandaa *calibration chart* ambayo huandaliwa na Afisa Vipimo ikioneshaa taarifa zifuatazo:-

- ✓ Ujazo wa gari
- ✓ Jina la mmiliki wa gari
- ✓ Namba ya gari
- ✓ Kiasi cha ujazo wa kila chumba (*compartment*)
- ✓ Muhuri na tarehe ya gari kupimwa
- ✓ *Calibration* namba

Calibration chart husainiwa na kugongwa muhuri wa moto upande wa kulia chini pamoja na kugongwa muhuri wa Meneja wa Mkoa husika.

- ix. Mteja anatakiwa kufanya malipo na ataandikiwa risiti toka ofisi ya Wakala wa Vipimo baada ya kukamilisha malipo hayo

- x. Mwisho mteja anakabidhiwa *calibration chart* yake, stika pamoja na *dip stick*.

WAJIBU WA DEREVA ANAYESAFIRISHA MAFUTA

- ✓ Ni wajibu wa dereva kuleta gari lake kuhakikiwa kila muda unapofika ama linapokuwa limepata ajali au kama anaona halipo sahihi ili lije kwa ajili ya kulipima upya.
- ✓ Ni wajibu wa dereva kuleta *dip stick* pamoja na *calibration chart original* iliyokwisha muda wake.
- ✓ Ni wajibu wa dereva kuhakikisha gari lake ni zima na linakidhi vigezo vyote vinavyohitajika kwa ajili ya upimaji.

HAKI YA DEREVA ANAYESAFIRISHA MAFUTA

- ✓ Ni haki ya dereva anapoenda kupakia mafuka katika *depot* kuuliza kama *flow meter* ya kujazia mafuta imehakikiwa na Wakala wa Vipimo kwa mwaka husika na kuoneshwa uthibitisho wa *seal* ya Wakala wa Vipimo ikibidi.



Afisa Vipimo
akifanya uhakiki
wa *Flow Meter*
inayotumika
kujazia mafuta
kwenye Maroli.

- ✓ Ni haki ya dereva anapoenda kushusha mafuta kuuliza kama kisima cha kuhifadhiha mafuta (*Underground tank*) kimehakikiwa na Wakala wa Vipimo kwa wakati na kuoneshwa chati ikibidi.
- ✓ Ni haki ya dereva anapoenda kujaza mafuta kwenye kituo cha mafuta kuuliza kama pampu zimehakikiwa na Wakala wa Vipimo na apewe uthibitisho.
- ✓ Ni haki ya dereva kukabidhiwa *calibration chart*, sticker pamoja na *dip stick* mara baada ya gari kuhakikiwa na Wakala wa Vipimo.

Kwa mawasiliano zaidi;

**Afisa Mtendaji Mkuu, Wakala wa Vipimo,
Jengo la NSSF- MAFAO, Mtaa wa Uhuru, Ilala, Orofa ya Saba,
S.L.P 313, Dar es Salaam. Simu: +255 (022) 2928156,
Barua pepe: info@wma.go.tz, Tovuti: www.wma.go.tz**